MARIE STOPES
TANZANIA

# FAMILIA

Toleo Na: 9




*Tunabadili maisha, kila mwanamke kwa wakati*

MARIE STOPES TANZANIA

# Yaliyomo ndani ya Jarida



- Safari yetu katika kufikia malengo ya mwaka 2023
- Mwongozo wa taifa wa jumbe za Uzazi wa Mpango waidhinishwa na kuzinduliwa
- CAMMAC yawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria kwenye Tume ya Haki Jinai
- Wabunge vinara wa afya ya uzazi wafurahishwa na kutengenezwa kwa muswada wa sheria ya haki za afya ya uzazi
- Mafunzo ya Elimu ya Ujinsia kimtandao yatolewa kwa walimu na maafisa elimu kata Mkoani Morogoro
- Mfumo wa kuimarisha afya ya uzazi katika vituo vya serikali waendelea; Vifaa tiba katika Vituo vya afya vyatolewa
- Kliniki za mwisho wa wiki zaongeza upatikanaji wa taarifa na huduma za Afya ya Uzazi kwa vijana balehe
- Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2023
- Kitengo cha masoko chapiga hatua chanya
- Matukio katika Picha

# Safari yetu katika kufikia malengo ya mwaka 2023




Jumla ya Wateja waliofikiwa

**364,508**




Wateja waliotembelea vituo vyetu walio chini ya miaka 20

**69,148**




Alama za muda wa uzuiaji mimba (CYPs) zilizozalishwa

**1,086,350**



Mimba zisizotarajiwa zilizoepukwa

**1,422,431**



Utoaji mimba usio salama ulioepukwa

**319,552**

Chanzo: Ripoti ya robo mwaka Jan - Mar 2023

# Muongozo wa Taifa wa jumbe za Uzazi wa Mpango waidhinishwa na kuzinduliwa




Shirika la Marie Stopes Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na wadau wanaotekeleza miradi ya afya ya wamefanya mapitio ya Mwongozo wa Taifa wa Jumbe za Afya ya Uzazi wa mwaka 2003.

Mapitio ya Mwongozo huu ni matokeo ya juhudi za uchechemuzi ambao lengo lake ni kupitia miongozo iliokuwepo au kutengeneza miongozo mipya ya afya ya uzazi na kushirikisha watoa huduma na wadau katika ngazi zote ili kuimarisha ubora wa utoaji huduma za afya ya uzai.

Wizara ya Afya imehitimisha, kuhakiki na kusaini Muongozo huu ambao utasaidia watoa huduma za afya ya uzazi kuwa na taarifa na namna ya kuwasiliana na wateja ili kuweza kuwafikia wateja kwa urahisi na kuongeza matumizi ya uzazi wa mpango. Mwongozo huu umezinduliwa na Mratibu wa Uzazi wa Mpango taifa mnamo mwezi Januari mwaka 2023 ambapo mpango wa kuusambaza kwa wadau mbali mbali uliafikiwa. Katika tukio hili, Marie Stopes Tanzania iliwakilishwa na Mkuu wa kitengo cha ubora wa huduma za afya Dkt. Seleman Mbyallu.

# CAMMAC yawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria kwenye kamati ya Haki jinai



Kufuatia kuundwa kwa tume ya marekebisho ya sheria na haki jinai inayopokea maoni kwa lengo la kuboresha mifumo ya haki jinai, Marie Stopes Tanzania (MST) kupitia CAMMAC imewezesha uwasilishwaji wa mapendekezo yenye dhamira ya kurekebisha vifungu 150,151,152 na 230 vya kanuni ya adhabu vinavyozuia wanawake kupata haki ya afya ya uzazi kama ilivyoelezwa chini ya Itifaki ya Maputo.

Chapisho la mapendekezo liliwasilishwa katika tume na kundi la wanawake wanasheria 10 ambao ni washirika wa Chama cha Wanawake Wanasheria wanaohusika na Haki za Afya ya Uzazi ambao pia ni wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society). Baada ya uwasilishaji kwa njia ya maandishi katibu mkuu wa tume alithibitisha kupokea na kukaribisha uwasilishaji wa ana kwa ana ambao ulipangwa kufanyika mnamo mwezi Aprili 2023

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi ya Guttmacher kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Taasisi ya Taifa ya tafiti za kitabibu, vitendo vya utoaji mimba hatarishi vinachangia kati ya vifo vya uzazi nchini kwa asilimia 16-19. CAMMAC hutoa fursa kwa wadau wanaotekeleza miradi ya afya ya uzazi kufanya uchechemuzi juu ya haki za afya ya uzazi kwa lengo la kuondoa vifo hivi vinavyoepukika.

Tume hiyo inafanya kazi chini ya uenyekiti wa aliyekuwa Jaji Mkuu Mohammed Chande Othman, imepewa hadi Mei 30, 2023 kufanya kazi hiyo na kuwasilisha ripoti yake ya awali kwa Rais. Wajumbe wa tume hiyo ni pamoja na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Ombeni Sefue, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) Edward Hosea, aliyekuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS) Yahya Khamisi Hamad, aliyekuwa askari wa Jeshi la Polisi, Saada Ibrahim. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco), Omary Issa, Afisa Mwandamizi kutoka Ofisi ya Rais, Baraka Leonard, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Eliezer Feleshi, Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Dkt. Laurean Ndumbaro na waliokuwa Wakuu wa Jeshi la Polisi IJP Said Mwema na Ernest Mangu.



*Wanawake Wanasheria wanaojishughulisha na Haki za Afya ya Uzazi wakiwa katika picha ya pamoja na mmoja wa wajumbe wa Tume ya Rais ya Haki Jinai.*

# Wabunge vinara wa afya ya uzazi wafurahishwa na kutengenezwa kwa mswada wa sheria ya afya ya uzazi



Mnamo Januari 2023 CAMMAC walifanya mkutano na wabunge na kuwasilisha matokeo ya utafiti juu ya gharama baada ya mimba kuharibika iliopelekea wabunge kuomba kutengenezwa kwa muswada wa sheria wenye lengo la kuondoa vikwazo kwa wanawake kupata huduma za afya ya uzazi.

Mkutano huo uliofanyika mjini Dodoma ulioshirikisha wabunge 29 uliwezeshwa na wataalam kutoka Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi Tanzania (AGOTA) waliowasilisha kuhusu ukubwa wa tatizo la utoaji wa mimba usio salama Tanzania pia mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) aliwasilisha utafiti wa gharama za huduma baada ya mimba kuharibika.

Wabunge hao walitoka katika makundi mbalimbali ndani ya bunge ikiwa ni pamoja na wabunge kutoka Chama cha Wabunge wanaojihusisha na Idadi ya Watu na Maendeleo (TPAPD), wabunge vinara wa afya ya uzazi, wabunge kutoka kamati ya huduma za Jamii na Kamati sheria na katiba.

Sambamba na hayo, wana mtandao walipendekeza hoja na maswali mbalimbali yanayohusu ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ambayo yangewasilishwa bungeni na kwa serikali katika kikao cha bunge cha Mwezi wa Pili 2023.

MST imewezesha CAMMAC kwa kumleta mtaalamu wa sheria ambaye ameanza kutengeneza mswada wa sheria unaotegemewa kuwasilishwa bungeni mwaka huu.





# Mafunzo ya Elimu ya Ujinsia kimtandao yatolewa kwa walimu na maafisa Elimu kata Mkoani Morogoro




MST kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), UNESCO na TACAIDS iliendesha mafunzo ya wakufunzi wa wakufunzi wa mitaala ya elimu ya ujinsia (CSE) kwa walimu waliopo kazini 1,656 katika wilaya nane za Tanzania bara zikiwemo Wilaya nne kutoka mkoani Morogoro ambako mradi wa Youth4Health unatekelezwa.

Lengo kuu la mafunzo haya lilikuwa ni kuwawezesha walimu kutoa elimu ya ujinsia na afya ya uzazi (CSE) kwa vijana mashuleni. TET kwa kushirikiana na wadau wengine ilifanya marekebisho ya miongozo ya afya ya uzazi, UKIMWI, ukatili wa kijinsia ili kuzifikia shule za msingi na sekondari kwa urahisi kupitia njia za kidijitali zikiwemo simu za mkononi, vishkwambi na kompyuta.

Mafunzo yalihusisha washiriki 41 (walimu walioko kazini na maofisa elimu kata), mafunzo haya yalifanyika mwezi Machi katika awamu mbili. Mafunzo ya kwanza yalifanyika Morogoro (katika Kituo cha Rasilimali za Walimu- TRC na washiriki kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Gairo huku mafunzo ya pili yalifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi (Kituo cha Ualimu cha Malinyi na washiriki kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi na Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga. .

Walimu waliopata mafunzo kama wakufunzi wa wakufunzi wanatarajiwa kutoa mafunzo yanayopatikana katika Mfumo wa Usimamizi wa Elimu wa Taasisi ya Elimu Tanzania kwa walimu wengine ndani ya shule zao na kata husika kupitia majukwaa yao ya Maendeleo Endelevu ya taaluma ya walimu katika jumuiya zao za kujifunza kila wiki.



# Mfumo wa kuimarisha afya ya uzazi katika vituo vya serikali waendelea: Vifaa tiba katika Vituo vya afya vyatolewa

Mwezi Februari 2023, MST kupitia mradi wa Youth4Health unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya ilitoa vifaa tiba kwa vituo 21 vya afya vya umma katika wilaya nne za mkoa wa Morogoro ili kuwezesha utoaji wa huduma za afya ya uzazi .

Katika hafla ya makabidhiano ya vifaa kwa timu ya menejimenti ya afya ya Mkoa wa Morogoro, Mganga Mkuu wa Mkoa aliishukuru MST na Umoja wa Ulaya kwa kutoa msaada wa vifaa kwa vituo hivyo.

“Vifaa hivi ni muhimu na vinahitajika sana kusaidia kushughulikia hitaji ambalo halijafikiwa la upangaji uzazi, sio tu kwa vijana bali pia kwa watu wazima. Nitafuatilia ili kuhakikisha vifaa vimefika kwenye vituo husika kwa wakati ili kuepusha ucheleweshaji wa utoaji huduma” alisema Mganga Mkuu.

Youth4Health ni mradi wa miaka mitatu wa unaolenga kuongeza wigo wa ufikiaji huduma za afya ya uzazi na haki kwa vijana kwa kuzingatia kufikia wasichana ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu maeneo ya vijijini na yasiyofikika kwa urahisi. Na pia kuongeza ufikiwaji wa huduma za afya ya uzazi kwa kuimarisha sera, sheria na miongozo pamoja na utengaji bajeti. Mradi huu wa Youth4Health utaongeza upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi na haki kwa vijana balehe.






# Kliniki za mwisho wa wiki zaongeza upatikanaji wa taarifa na huduma za Afya ya Uzazi kwa vijana balehe




Katika robo ya kwanza ya 2023, MST imeshuhudia ongezeko la idadi ya vijana wanaopata huduma na taarifa za Afya ya Uzazi katika wilaya za Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro kutokana na kuendeshwa kwa huduma za kliniki za afya ya uzazi siku za Jumamosi mwishoni mwa kila mwezi. Ikilinganishwa na vipindi vilivyopita, watoa huduma katika vituo vya serikali vilivyo katika mradi wa uboreshaji huduma walirekodi wateja vijana wa rika barehe asilimia 25, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 6 kutoka robo ya nne ya 2022.

Katika kuongeza ufikiwaji wa taarifa na huduma za afya ya uzazi kwa vijana walio ndani na nje ya shule, mfumo huu uliundwa ili kusimamiwa na watoa huduma ndani ya vituo vinavyofadhiliwa Mfumo wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi katika vituo vya serikali kwa usaidizi wa Watoa huduma ngazi ya jamaii wanaofanya kazi ya kuhamasisha vijana kuhudhuria.

Muundo wa kliniki za wikendi unatumia mbinu ya elimu inayohusisha michezo ya vijana huku ikijumuisha elimu na huduma za Afya ya uzazi, ukatili wa kijinsia, pamoja na uchunguzi wa magonjwa ya zinaa na upimaji wa VVU.



# Maadhimisho yaSiku ya Wanawake Duniani 2023




Tarehe 8 Machi, MST iliadhimisha Siku ya kimataifa ya wanawake kwa kutoa msukumo wa kuipa kipaumbele sekta ya afya ya uzazi nchini Tanzania katika kufikia usawa wa kijinsia.

Katika kuadhimisha siku hii Mkurugenzi Mkuu V.S Chandrashekar alifanya mkutano na waandishi wa habari siku moja kabla ya kilele cha na kutoa wito wa kuendelea kukuza uwekezaji kuhakikisha upatikanaji wa haki za afya ya uzazi na kuondosha masuala ya ukatili wa kijinsia kupitia kuonesha matokeo ya kazi zilizofanywa na shirika Marie Stopes Tanzania kwa mwaka 2022.

MST pia iliratibu kongamano kwa njia ya mtandao kujadili mada inayohusu “Kuendeleza usawa kupitia upatikanaji wa haki za afya ya uzazi” Mdahalo huo wa mtandaoni ulihudhuriwa na watu 589 na kushirikisha wadau mbalimbali kutoka Wizara ya Afya, Chama



cha Madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake (AGOTA), mwanasheria kutoka WGNNR, na mshauri wa masuala ya usawa wa kijinsia kutoka Marie Stopes Tanzania.

Sambamba na hayo MST iliadhimisha siku hii kwa kuendesha kampeni ya mtandaoni katika vyombo vya habari vya kidijitali ili juu ya kuhusu afya ya uzazi. Kupitia kampeni hii mitandao ya kijamii ilipata wafuasi wapya 7,161 kwenye Instagram, Twitter, Facebook, LinkedIn na clubhouse ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 5.3%. Pia washawishi wa mitandao ya kijamii walichapisha jumbe 103 zinazohusu haki za Afya ya Uzazi na usawa wa kijinsia na kuwafikia takriban watu milioni 4.9.

Timu ya wafanyakazi wa Marie Stopes Tanzania iliadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kusikiliza simulizi za moja kwa moja za watoa huduma katika nyanja hiyo kuhusu athari za kuhakikisha wanawake wanapata haki ya uzazi na namna hii ilivyowawezesha kuwa na sauti na nguvu katika maisha yao.

Akizungumza wakati wa hafla ya wafanyakazi, Mkurugenzi wa MST nchini V.S Chandrashekar aliipongeza timu hiyo kwa kazi wanayofanya kuhakikisha wanawake wanaweza kupata huduma kwa uhuru na taarifa sahihi na kwamba shirika linathamini mchango huo na si siku ya wanawake tu bali ni siku zote.



# Kitengo cha masoko chapiga hatua chanya







Katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza, MST iliendelea kuwekeza kwa kuongeza wigo wa masuala ya afya ya uzazi kwa kutoa elimu na kuuza bidhaa muhimu za afya ya uzazi kupitia mtandao wa masoko na kituo cha mawasiliano. Lengo ni kupanua chaguzi za afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana. Timu zetu za mauzo ziliweza kuuza kondomu za Lifeguard 520,000 na vidonge vya Misoclear 292,000.

Kupitia kituo chetu cha mawasiliano tumepokea zaidi ya simu 2,868 na kupokea jumbe za moja kwa moja zipatazo 5,192 kupitia chaneli zetu za mitandao ya kijamii ambayo ilisababisha rufaa 770 kwa zahanati na hospitali zetu. Mada kuu zilizoongelewa zilikuwa juu afya ya uzazi na upimaji wa magonjwa ya ngono ikifuatiwa na masuala ya uzazi wa mpango pamoja na huduma za uzazi.

Ili kufikia malengo katika mauzo MST ilifanya kazi na msanii wa muziki wa kizazi kipya maarufu kama G-Nako ambaye pia ni mshawishi wa mitandao ya kijamii iliopelekea mitandao yetu ya kijamii kuvutia watu 25,127 na kuzalisha wafuasi wapya 396. Kwa jumla, katika robo hii, ukurasa wa Lifeguard ulifikia karibu watu 54,231.

Mbinu hii ya masoko inasaidia kupanua ufikiaji wa watu wengi na kuhakikisha ubora wa huduma kwa mteja ambayo huleta uendelevu katika masoko na biashara .







# Matukio katika picha



*Picha mbalimbali za matukio ya maadhimisho ya hapa MST katika Siku ya Wanawake Duniani 2023*

# Matukio katika picha






*Picha mbalimbali za kikaocha mashauriano na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kilichohusu upatikanaji wa haki za afya ya uzazi*

MARIE STOPES
TANZANIA

# Matukio katika picha



*Picha ya pamoja ya wadau walioshiriki katika kikao kazi cha kutengeneza mpango wa mwaka wa Kitengo cha Uhamasishaji, Wizara ya Afya*




*Dkt Mashingo (kushoto) akiwasilisha mada katika kongamano la Vijana na Afya ya Uzazi lililoratibiwa na YUNA.*